# MAFUNDISHO YA BIBLIA

**kwa WATOTO wa**

**KANISA LA ELOHIM (COG)**

**SikuYa Saba (7th day)**

**————**

**Robo Ya Tatu**

**2023**

**—————**

**Ya**

**Julai, Agosti na Septemba**

**Kutumiwa na Biblia**

**—————**

**Watenda kazi wanahitajika, Mavuno ni mengi, Lakini watenda kazi ni wachache...**

**—————**

**Tuma maombi yote kwa,**

**3RD ANGEL MESSENGER**

**S.L.P. 9774**

**NAKURU.**

**3rdangelmessenger@gmail.com**

**SIMU: +254 721576325/+254 780976325**

**SOMO LA WATOTO LA JULAI 1,2023.**

**UUMBAJI**

**Somo kuu: Mwanzo 1:1-31**

**Fungu la kukariri: Mwanzo 1:1**

1. Nani aliziumba mbingu na nchi? Mwanzo 1:1.

2. Nini Elohim aliumba siku ya kwanza? Mwanzo 1:4-5.

3. Nini Elohim aliumba siku ya tatu? Mwanzo 1:9-13.

4. Ni-lini Elohim alimuumba mwanadamu? Mwanzo 1:26-31.

5. Baada ya uumbaji, Elohim alifanya nini ? Mwanzo 2:1-2.

6. Je,Elohim alipumzika baada ya uumbaji kwa kuwa alikuwa amechoka? Isaiya 40:28 upatanishe na Kutoka 20:8.

7. Nina aliwapea wanyama Majina yao baada ya uumbaji? Mwanzo 1:20.

**SOMO LA WATOTO LA JULAI 8,2023.**

**BIBLIA**

**Somo kuu: Zaburi 119:105-115**

**Fungu la kukariri: 2 Timotheo 3:16**

1. Nini faida ya neno la Elohim katika maisha yetu? Zaburi 119:105

2. Nabii Yeremia alinena vipi kubusu neno la Elohim? Yeremia 15:16

3. Je,tumeshauriwa tujifunze neno la Elohim? 2 Timotheo 2:15

4. Kulingana na Mtume Paulo, nini kinafaa kuwa kwa wingi ndani ya roho zetu? Wakolosai 3:16

5. Neno la Elohim lime-elezewa vipi? Yohana 1:1

6. Neno la Elohim lilianza lini? Yohana 1:2

7. Je, kuna Baraka inayopatikana kwa kuyashika maneno ya Elohim? Ufunuo 22:7

**SOMO LA WATOTO LA JULAI 15,2023.**

**KUZALIWA KWA MASIHI**

**Somo kuu: Luka 2**

**Fungu la kukariri : Luka 2:52**

1. Je,manabii walijua Mahali ambapo Masihi angezaliwa? Mika 5:2,Mathayo 2:5
2. Nani alitaka kumuua Masihi? Luka 2:1
3. Nani alikuwa mama yake? Mathayo 1:18
4. Kwa nini Masihi na wazazi wake walienda Misiri? Mathayo 2:13-14
5. Ni lini walirudi kutoka Misiri? Mathayo 2:19-21
6. Ni katika Mji upi waliishi baada ya kutoka Misiri? Mathayo 2:23
7. Katika utotoni wake, je alikuwa ana watii wazazi wake na Elohim? Luka 2:52

**SOMO LA WATOTO LA JULAI 22,2023**

**HUKUMU**

**Somo kuu: Ufunuo 20**

**Fungu la kukariri : 2 Wakorinitho 5:10**

1. Je,kutakuwa na hukumu kwa watu wote? 2 Wakorinitho 5:10
2. Hukumu inaanzia wapi? 1 Petero 4:17
3. Je,siri zote njema na mbaya zitaletwa mbele ya hukumu? Mhubiri 12:14
4. Je,maneno yetu yatahukumiwa? Mathayo 12:36
5. Imesemwa vipi kuhusu malaika walioanguka kutoka mbinguni? Yuda 1:16
6. Imesemwa vipi kuhusu hukumu katika Waraka Waibrania? Waibrania 9:27
7. Je,Mataifa wataiona hukumu ya Elohim? Ezekieli 39:21

**SOMO LA WATOTO LA JULAI 29,2023.**

**UZIMA WA MILELE**

**Somo kuu: Yohana 17**

**Fungu la kukariri : Yohana 3:16**

1. Ni kwa nini Elohim alimtuma mwanawe wake aje ulimwenguni? Yohana 3:16

2. Nini ahadi ya Masihi kwetu? 1 Yohana 2:25

3. Je, mtu anaye waua wengi e ana uzima wa milele? 1 Yohana 3:15

4. Ni swali gani mtu moja alimuuliza Masihi kuhusu uzima wa milele? Mathayo 19:16

5. Jibu la Masihi, lilikuwa lipi? Mathayo 19:17

6. Tukimuamini Masihi, je tutapata uzima wa milele? 1 Yohana 3:15

7. Nini karama ya Elohim kwa waliomwamini? Warumi 6:23.

**SOMO LA WATOTO LA AGOSTI 5,2023.**

**MAOMBI**

**Somo kuu: Mathayo 6:1-21**

**Fungu la kukariri : 1 Wathesalonike 5:17**

1. Ushauri wa Paulo kuhusu maombi ni upi? Wakolosai 4:2,1 Wathesalonike 5:17

2. Tuombapo tumeshauriwa tufanye vipi? 1 Wakorinitho 14:15

3. Je, Paulo aliwaambia ndugu wengine wamkumbuke katika maombi Yao? Wakolosai 4:3

4. Je,Danieli aliogopa kuomba Elohim baada ya mfalme kutoa agizo la kwambai mtu yeyote

asimuombe Elohim? Danieli 6:10

5. Ni ombi lipi Masihi aliwafunza wafuasi wake? Mathayo 6:9-13

6. Tunapo omba nini tumeshauriwa tusifanye? Mathayo 6:5-6

7. Je,Elohim huyasikia maombi ya watakatifu? 1 Peter 3:12.

**SOMO LA WATOTO LA AGOSTI 12,2023.**

**DANIELI**

**Somo kuu: Danieli 1**

**Fungu la kukariri : Danieli 1:6**

1. Danieli alikuja vipi katika nchi ya walikadayo? Danieli 1:1-4.

2. Ni nani wengine walichaguliwa pamoja naye iliwafunzwe lugha ya walikadayo? Danieli 1:4, 6.

3. Ni majina yapi walipewa na Mkuu wa matowashi? Danieli 1:7.

4. Je, Danieli alipendwa na Elohim zaidi? Danieli 10:11.

5. Nini imesemwa kuhusu Danieli na Nabii Ezekieli? Ezekieli 14:14; 14:20; 28:3.

6. Nini Masihi aliwakumbusha wafuasi wake kuhusu unabii wa Danieli? Mathayo 24:15.

7. Je,Danieli alikuwa akiomba Elohim kila wakati? Danieli 6:10.

**SOMO LA WATOTO AGOSTI 19,2023.**

**YERUSALEMU**

**Somo kuu : Isaya 62:12**

**Fungu la kukariri : Zaburi 147:2**

1. Ni Mahali gani Elohim alipachagua kuliweka Jina lake? 2 Mambo ya Nyakati 6:6

2. Je,tumeshauriwa kuiombea Yerusalemu? Zaburi 122:6

3. Ni vipi Nabii Isaya amenena kuhusu Yerusalemu? Isaya 24:23

4. Ni nini kilifanyika Kwa wakaaji wa Yerusalemu walipotenda uovu? Yeremia 32:32-36

5. Nini kilifanyika baada ya kutekwa mateka, je baadaye walirudishwa Yerusalemu? Yeremia

32:37

6. Ni Mahali gani wanafunzi wa Masihi walianza kuhubiri injili? Luka 24:47

7. Yohana wa ufunuo amenene vipi kuhusu Yerusalemu mpya? Ufunuo 21:2, 21:10

**SOMO LA WATOTO LA AGOSTI 26,2023.**

**MUSA**

**Somo kuu : Kutoka 2:1-25**

**Fungu la kukariri : Kutoka 2:10**

1. Jina Musa humaanisha nini? Kutoka 2:10

2. Ni katika kabila ipi, wazazi wa Musa walitokea? Kutoka 2:1-2

3. Musa alipotelea wapi, alipotoroka Misiri? Kutoka 2:15

4. Jina la Mke wa Musa kutoka kwa kuhani wa Wamediani lilikuwa lipi? Kutoka 2:21

5. Mwanawe aliitwa Nani? Kutoka 2:22

6. Nani alikuwa Baba yake Musa? Kutoka 6:20

7. Je,Musa alikuwa mnyenyekevu? Hesabu 12:3

**SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 2,2023**

**PETERO YULE MTUME**

**Somo kuu : Mathayo 10:1-12**

**Fungu la kukariri : Mathayo 10:2**

1. Nani alikuwa ndugu ya Petero na Mtume wa Masihi pia? Mathayo 4:18

2. Katika wale mitume kumi na wawili wa Masihi na alijua Masihi ni mwana wa Elohim?

Mathayo 16:16

3. Nani alimfunulia Petero ya kwamba, Masihi ni mwana wa Elohim? Mathayo 16:17

4. Jina la Petero lingine lilikuwa lipi? Marko 3:16

5. Je,Petero alikubali watu wamuinamie? Matendo ya Mitume 10:25-26

6. Je, Petero aliwekwa korokoroni kwa sababu ya injili ya Masihi? Matendo ya Mitume 12:1-5

7. Je,Elohim alimtoa kutoka korokoroni? 12:7-11

**SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 9,2023.**

**YOHANA YULE WA UFUNUO**

**Somo kuu : Ufunuo 1:1-20**

**Fungu la kukariri : Ufunuo 1:9**

1. Nani alipewa Ufunuo wa Masihi? Ufunuo 1:1

2. Je,Yohana alikuwa mmoja wa wale mitume kumi na wawili wa Masihi? Mathayo 4:21, 10:2

3. Nani alikuwa baba yake? Mathayo 4:21

4. Baada ya Masihi kupaa mbinguni, je Yohana alikuwa baadhi ya Mitume wale watatu waliokuwa Nguzo ya Kanisa? 2:9

5. Ni ushahidi upi mwingine ambao waonyesha kuwa Ufunuo ulipewa Yohana? Ufunuo 1:14

6. Nani alimuuwa Ndugu yake Yakobo? Matendo ya Mitume 12:1-2

7. Ni jambo gani lilifanyika wakati Petero na Yohana walipoenda kuomba katika hekalu? Matendo ya Mitume 3:1-11

**SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 16,2023.**

**YOHANA MBATIZAJI**

**Somo kuu : Mathayo 3:1-17**

**Fungu la kukariri : Mathayo 3:1**

1. Ni Nani walikuwa wazazi wa Yohana Mbatizaji? Luka 1:13

2. Je alikuwa ametabiri kuhusu Masihi? Luka 3:16

3. Je,alimbatiza Masihi? Mathayo 3:13-16

4. Alipokuwa nyikani, alikula nini? Marko 1:6

5. Je,Yohana alifungwa jela? Marko 6:17

6. Nini ilikuwa sababu ya Yohana kufungwa jela? Marko 6:18-19

7. Nini kilifanyika katika jela, je alitoka kutoka jela? Marko 6:21-29

**SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 23,2023.**

**MJI ULE MTAKATIFU (YERUSALEMU MPYA)**

**Somo kuu : Ufunuo 21:1-22**

**Fungu la kukariri : Ufunuo 21:2**

1. Nani aliona Mji ule mtakatifu ukishuka duniani? Ufunuo 21:2

2. Ni milango ngapi itakuwa katika Mji ule mtakatifu? Ufunuo 21:12

3. Ni lipi jina la mji wa Elohim? Ufunuo 3:12

4. Je,mwandishi wa waraka wa waebrania alinena kuhusu mji huu? Waebrania 13:14

5. Nani Mjenzi wa mji huu? Waebrania 11:10

6. Ni nini kinahitajika ili mtu aingie katika mji mtakatifu? Ufunuo 22:14

7. Je,watu waovu wataingia katika mji mtakatifu? Ufunuo 21:27;22:15

**SOMO LA WATOTO LA SEPTEMBA 30,2023**

**NYAMA SAFI NA NYAMA ISIYO SAFI**

**SomoKuu: Walawi11:1-23**

**FunguLa Kukariri: Walawi20:25**

1. Je, tumekubaliwa kula kila Nyama? Walawi 20:25

2. Isopokuwa katika kitabu cha Walawi, nimahali pengine wapi tunapata jambo hili?

Kumbukumbu la torati 14:3-20

3. Nabii Isaya amesema vipi kuhusu watu wanaokula nyama najisi kama Nguruwe naPanya?

Isaya 66:17

4. Katika agano jipya jambo hili limenenwa vipi? 1 Tomotheo 4:4-5

5. Nuhu aliamriwa aje kuhusu jambo hili? Mwanzo 6:21

6. Nuhu alifuata amri hii? Mwanzo 8:20

7. Je, twafaa kufuata jambo hili? Warumi 15:4